



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA
SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)



HALMASHAURI YA MANISPAA YA
MOSHI

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na.MMC/B.10/3 VOL.III/118

Tarehe : 18/05/2023

**TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA YA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI KWA KIPINDI
CHA MWAKA 2023 HADI 2026**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi anawatangazia Wananchi kuwa kuna nafasi wazi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira ya Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kwa kipindi cha miaka mitatu 2023 hadi 2026.

SIFA ZA MWOMBAJI:

1. Awe ni raia wa Tanzania na mkazi wa Moshi.
2. Awe na angalau Shahada ya Kwanza katika fani za Utawala, Sheria na Sayansi ya Jamii.
3. Awe na akili timamu.
4. Asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai
5. Asiwe na Wadhifa wa Kisiasa au Uongozi wa ngazi yoyote katika Chama cha Siasa.
6. Awe Mtumishi wa Umma.

TARATIBU ZA KUWASILISHA MAOMBI

Waombaji wote watume barua za maombi zikiwa na viambatisho vifuatavyo:-

- i) Nakala iliyothibitishwa ya cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha Taifa (Certified copy).
- ii) Nakala zilizothibitishwa za vyeti vya masomo na Taaluma (Certified Copies).
- iii) Barua ya utambulisho toka kwa Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa anapoishi. Ikiwa na picha ndogo ya hivi karibuni.
- iv) Wasifu binafsi (CV).
- v) Barua toka kwa Wadhamini wawili (2) zikiwa na Anuani kamili na Email.

NB: Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 16 Juni, 2023 saa 9:30 Alasiri.

Barua zote za maombi zitumwe kwa anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi wa Manispaa,
S.L.P 318,
Halmashauri ya Manispaa,
MOSHI.**


Mkurugenzi wa Manispaa
Moshi
Sifael Tuluwene Kulanga
KAIMU MKURUGENZI